



Mimea Vamizi Afrika Mashariki


Kutathmini na kukabiliana na athari zake kwenye mazingira na maisha

<http://www.woodyweeds.org/>

Madhara ya Promi (Prosopis) kwenye maisha ya watu wa kaunti ya Baringo na usimamizi endelevu wa ardhi ili kukabiliana na athari zake




Mti wa Promi uliletwa katika maeneo makavu ya Africa Mashariki katika miaka mwisho mwisho ya 1970 kupunguza uharibifu wa udongo na kumaliza uhaba wa kuni. Promi hutoa chakula ya mifugo, kivuli, kutengeneza ua, kuni na mapato ya pesa kwa kuchoma makaa.



"Mimi ninasoma na wanafunzi na kufanya kazi na wataalamu kutoka nchi mbalimbali ili kuweza kutusaidia kuelewa zaidi na kudhibiti shida ya Promi na kulinganisha hali ilivyo katika Kenya na nchi zingine zilizo adhirika na mti huu."

Purity Rima ni Wanafunzi wa shahada ya PhD katika Chuo Kikuu cha Nairobi na KEFRI

Katika Kaunti ya Baringo, Promi imesambaa maeneo mengi ambako inaleta uharibifu wa: miiba yake humiza watu na wanyama; kuharibu malisho; kupunguza uwezekano wa kupata lishe ya mifugo na maji; hupunguza mimea na wadudu wa kiasili pamoja na kuongeza gharama ya utunzaji wa ardhi.



Tunaonyesha kwa ramani za Satellite maeneo ambayo tayari yamevamiwa na Promi katika Afrika Mashariki na maeneo ambayo yapo katika hatari ya kuvamiwa na mti huu kwa miaka ijayo. Tunachunguza madhara ya mti huu kwa mazingira, watu na uchumi. Tunaangalia jinsi madhara haya ubadilika wakati ambapo eneo lililovamiwa, Promi itazidi kuongezeka.

Katika Kaunti ya Baringo, tunaangalia jinsi kusambaa kwa Promi kunachangiwa na kutembea kwa binadamu na wanyama, na uvyausaji (hybridization) wa Promi iliyopandwa mwanzo. Pia tunachunguza huhusiano wa Promi na kuhifadhi carbon iliyo chini ya ardhi, ambayo itaweza kuwa muhimu kwa upunguzaji makali ya kubadilika kwa hali ya anga.



Mradi wetu utanufaisha wanavijiji (jamii), Makundi yasio ya kiserikali (NGOs), na mashirika mamlaka ya kiserikali, kuchagua mbinu bora za utunzaji Promi ili kupunguza madhara mabaya na kuwezesha kupata manufaa makubwa kutokana mti huu. Kwa sababu hiyo, tutapima na kutenga visehemu vidogo vya ardhi kuonyesha jinsi ya kutunza Promi na kurejesha maeneo mazuri ya nyasi.

Kwa taarifa zaidi ongea na: Simon Choge, KEFRI Baringo, Marigat: Tel. +254 722 862 366



Swiss Programme for Research
on Global Issues for Development



Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Swiss Agency for Development
and Cooperation SDC

